



## SWALA KWA AJILI YA UBINADAMU.

ndugu zetu Waumini wa Mwenyezi Mungu Muumba, ndugu zetu katika ubinadamu sehemu yeyote...

Leo hii ulimwengu wetu unakumbwa na hatari kubwa inayotishia maisha ya mamilioni ya watu ulimwenguni, kwa sababu ya kuenea haraka kwa virusi vya corona “covid-19”, kwa imani yetu sisi tunasisitiza umuhimu wa duru ya tiba na utafiti wa kisayansi katika kupambana na janga hili bila kusahau kumuelekea Mwenyezi Mungu Muumba katika tatizo hili kubwa, hivyo basi tunatoa wito kwa watu wote sehemu zote duniani wamuelekee Mwenyezi Mungu kwa swala, vitendo vya kheri na unyenyekevu pamoja na maombi, kila mmoja sehemu yake kwa dini yake imani yake au dhehebu lake ili Mwenyezi Mungu aondoe janga hili na kutunusuru nalo na kuwapa nguvu wasomi ili kugundua dawa itakayo tokomeza ugonjwa huu na kuuokoa ulimwengu na matokeo mabaya ya kiafya kiuchumi na kiutu kutokana na kuenea kwa janga hili hatari.

Kamati Kuu ya kufikia malengo ya waraka wa undugu wa kibinadamu siku ya alhamisi ya tarehe 14 ya mwezi wa tano unaokuja inapendekeza iwe ni siku ya swala na maombi kwa ajili ya ubinadamu, na Kamati inatoa wito kwa viongozi wote wa kidini na watu wote duniani kuitikia pendelezo hili la kiutu na kibinadamu na kumuelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa sauti moja ili kulinda ubinadamu, na asaidie kwenye kushinda janga hili na kurejesha amani utulivu afya na maendeleo ili ulimwengu wetu baada ya janga hili ufungamane zaidi na ubinadamu na undugu kuliko wakati wowote uliopita.

Kamati Kuu ya undugu wa ubinadamu.